Na Dk Vicent Anney

Madhara ya uvuvi haramu na hatua mujarabu kuudhibiti

Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan akishiriki katika kuchoma nyavu zinazotumika katika uvuvi haramu.

JANA tulianza kuangalia sababu takribani 10 za uvuvi haramu kutoisha Ziwa Victoria. Baadhi ya sababu hizo ni rushwa, ufinyu wa bajeti ya kusimamia uvuvi, upungufu wa rasilimali watu, ushiriki mdogo wa wananchi katika vita dhidi ya uvuvi haramu, kuingia ziwani kuvua bila taratibu na baadhi ya wanasiasa kukingia kifua wavuvi haramu.

Lakini sababu kubwa ya uvuvi haramu tuliona kuwa ni wananchi kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu madhara ya uvuvi haramu na hivyo kuamini kuwa wenkali inawaonea kwamu uvuvi wanaofanya ni avili yao tangu zamani.

Katika makala haya leo tunaangalia madhara ya uvuvi haramu kwa mareo ya maziwa makuu ya Tanzania na mambo tunayoweza kufanya ili kumaliza tatizo la uvuvi haramu nchini.

Madhara ya uvuvi yanasababisha kupungua sana kwa samaki ziwani na kutoweka wapatikane kwa shida. Hali hii husababisha bei ya samaki kupanda na wengi kushindwa kuwanunua.

Sambamba na hilo viwanda vya samaki huwa katika hatari ya kufa na mimi nimeona uvuvi haramu ukiendelea licha ya juhudi zinazochukuliwa, muda si mrefu viwanda hivi vitakuta katika maeneo yote ya Ziwa Victoria.

Katika wilaya ya Musoma kwa mfano, kwa sasa kati ya viwanda vinne ni kimoja tu kinachofanya kazi.

Taarifa zilizopo zinaonesha pia kwamba nchini Marekani katika ukanda wa maziwa makuu ya Ontario, Michigan na Huron, viwanda vya samaki vilianza kupungua sana katika miaka 1860 kutokana na uvuvi haramu na vikafa kabisa ilipofika mwaka 1899. Na leo hii imebaki historia tu, hakuna viwanda vya samaki katika maziwa hayo.

Pili, umeskini uta-ongezeka sana maeneo ya pembezoni mwa ziwa kwa ukosefu wa ajira inayotokana na uvuvi. Kama nilivyoeleza katika makala iliyopita, shughuli za uvuvi zimeajiri aina mbalimbali za watu, hivyo kukosekana kwa samaki kutafanya Ziwa Victoria kutokuwa na maana kwa jamii.

Tatu, kufa kwa sekta ya uvuvi kutaongeza tatizo la uhalifu mtaani kutokana na vijana walokosa kazi kutafuta namna ya kuishi kwa kufanya upambazi. Kimsingi, uvuvi mdogomdogoni ni uhai wa maziwa katika nchi na amani kwa Taifa.

Hatua za kuchukua

Kwa mawazo yangu, kwa kuzijua sababu za uvuvi kuendelea kudumu katika Ziwa Victoria licha ya juhudi zinazochukuliwa, kunatupa mwanga wa kuona nini chakufanya kwa kufanyia kazi sababu hizo.

Kuna hatua kadhaa ambazo zinatakiwa kuchukuliwa katika harakati za kumaliza kabisa tatizo la uvuvi haramu Ziwa Victoria na hata kwenye maziwa mengine na mito na hata kwenye bahari. Pengine kuraweza kuwa na hatua zingine lakini hizi baadhi ya hazo.

Mosi ni kushirikisha jamii katika kusimamia rasilimali za uvuvi. Licha ya tatizo mbalimbali za maziwa makuu nchini Tanzania kuonesha kuwa jamii inaona hakuna uvuvi haramu, elimu nyingi inahitajika zaidi kwa mpa shirikishi ambayo itaitanya jamii kuamini kuwa kuna uvuvi haramu ambao unaangamiza kuendelea kuwepo kwa kizazi cha samaki katika ziwa hilo.

Ni muhimu wananchi wajue kwa undani madhara ya uvuvi haramu katika kumuhisa samaki ziwani ikiwemo kuua mayai, vifaranga au kuharibu mazalia ya samaki. Uvuvi haramu ni pamoja na matumizi ya nyavu zenye matundu madogo pamoja na makokoro, uvuaji wa kutumia sumu, mabomu au kutumia nyavu za timba.

Hatua ya pili ninayopendekeza ni kuanzisha ushuru wa samaki (fish levy) ili kugharamia doria za mara kwa mara na kuwalipa viongozi wa BMU ili wasaidie kuwa walinzi halisi wa rasilimali za majini.

Tukianzisha ushuru huu, kwa mfano kwa kila kilo moja inayouzwa tunaweza kupendekeza Sh 50 tu ambayo maeneo katika sekta ya samaki.

Itasaidia kununua mafuta ya boti za kufanya doria, posho za BMU na fedha kwa ajili ya matumizi ya ziezi la ukaguzi.

Tatu, kusimamia, kuvidahamu na kuvisajili vyombo vyote vya uvuvi katika maeneo ya maziwa makuu ya Tanzania. Tatizo linalochangia uvuvi haramu ni kukosekana kwa takwimu halisi za vyombo na vifaa vinavyotumika katika uvuvi. Yaani ni nani anavua kasi gani.

Maziwa ya Tanzania yameptakana na nchi mbalimbali hivyo usimamizi wake unahitaji nguvu ya pamoja. Shirika la Chakula Duniani (FAO) limewahi kuripoti kuwa uvuvi haramu unaripotiwa unahaki tishio kwa maendeleo ya bahari, maziwa na mito kwa sababu unadhoofisha jumuda za kimataifa na kimaeneo katika kulinda rasilimali za majini zisipotee.

Katika Ziwa Victoria upande wa Tanzania kuna bahari za wavuvi wanaotoka Kenya, Uganda na hata wengine kutoka Rwanda, Burundi hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Congo. Wanavua na kuvufaika na rasilimali za Tanzania sawa hi na Watanzania?

Nne, ni kuanzisha utaratibu ambao kila mvuvi lazima anapoingia ziwani anaazia kwenye mwalo na anapotoka kuvua lazima 'agoe' kwenye mwalo akiwa na vifaa na samaki alioavvua. Mfumo au utaratibu huu utasaidia katika kumarisha usimamizi, ukaguzi na ukusanyaji wa mapato ya samaki.

Mvuvi akifika kwenye mwalo anapotoka ziwani, samaki wake wanatakiwa kupimwa na kupewa kibali na ofisa uvuvi. Samaki wote wanaopelekwa sokoni lazima wawe wamepata kibali kutoka kwa afisa uvuvi na wawe wamekidhi viwango kama ilivyo kwa mabucha ya nyama.

Katika nyama, lazima mabucha yakaguliwe na nyama lazima ipate kibali cha daktari wa mifugo kabla ya kuuzwa buchani.

Hatua ya tano ni kufanyia mabadiliko idara za uvuvi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi za mikoa kuwa na sura bora zaidi kuliko ilivyo sasa, sawa na usimamizi wa misitu na wanyama pori unavyofanyika.

Kwa mfano, baada uwepo wa tatizo la ujangili wenkali iliarizisha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kwa ajili ya kupambana na ujangili kwenye sekta wanyama pori na hivyo hata kwenye sekta ya uvuvi kuna ujangili pia na hivyo kunahitajika chombo maalumu kama hicho.

Chombo hiki kitakuwa na wajibu pia wa kuelemisha jamii ili kujua kwamba kuna uvuvi haramu na unathari nyingi hasi katika maendeleo endelevu ya mazao ya samaki.

Wengi wa maofisa uvuvi uzalendo umekuwa mdogo na kujihusisha na rushwa na pengine kukiundwa chombo maalumu kama TAWA au Wakala wa Misitu (TFS) itasaidia katika kulinda rasilimali hizi.

Kimsingi, lengo kuanzisha jeshi usu uo kuwatisha watanzania bali kulinda rasilimali za majini na hata kuwalinda wavuvi wenyewe dhidi ya wezi wa nyavu na maharamia wengine wa majini.

Hatua ya sita ninyopendekeza ni kusimamia sheria ya uvuvi kwa kuiboresha hasa kwa kuzuia uagizaji na utengenezaji wa zana haramu za uvuvi nchini.

Pamoja na kwamba tunayo sheria ya uvuvi adhabu yake ni ndogo kuliko uharibifu unaofanywa na matumizi uvuvi haramu.

Sheria iliyopo inapelekeza zaidi katika utaifishaji wa mali za wavuvi haramu.

Hatua ya saba kuunganisha pamoja idara za ulinzi na usimamizi wa rasilimali za samaki za ngazi ya halmashauri na mikoa au kanda ili kuwa na mpangu kazi endelevu na wa pamoja na kuondoa hali ya kutegeana au kuingiliana majukumu. Hivi sasa sasa kila upande una mipango yake.

Nane, maeneo ya mazalia ya samaki yatambuliwe na kulindwa ili kuwepo kwa uvuvi endelevu katika eneo zima la maziwa makuu.

Nasuavyo mimi bado kama tasla hatujajipanga kutumia uvuvi kama kichocheo cha maendeleo. Nimeona hata katika ilani ya CCM serikali imepanga kuitumia sekta ya uvuvi kama eneo moja wapo litakalochangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi (uk. 5).

Tunaposoma utekelezaji wa ilani ya CCM 2020 – 2025 – ambayo imeelekeza katika uzalishaji unaongezeka katika mazao ya chakula, mifugo na uvuvi kwa ajili ya kuptosheleza kwa chakula na lishe bora ni vyema uvuvi haramu ukapigwa vita sana na kila mtanzania.

Mwandishi wa makala haya ni Mkuu wa Wilaya ya Musoma na mchangiaji wa gazeti hili.

Scanned with CamScanner

JUKWAA LA UCHUMI

MV ILEMELA
Ukuja-kuku wa usafiri wa majini katika mikoa ya kanda ya ziwa una umuhimu mkubwa... UK.13+12

Ukuaji sekta ya ngozi utakavyotafsiri maisha ya mfanyabiashara na mfugaji

MKURUGENZI wa Woiso Original Products Keneth Woisso aliyesimama akikagua ubora wa viatu vya ngozi

Na Gift Mongi.

TAKWIMU kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi asilimia 62 ya wakazi wa vijijini na 23 ya wakazi wa mijini wanafuga aina mbalimbali za mifugo; ikiwemo kuku, mbuzi, ng'ombe, nguruwe na mifugo mingine.

Wastani wa ng'ombe ni milioni 33.4 , mbuzi milioni 21.3, kondoo milioni 5.6 , nguruwe milioni 2.1 milioni, punda milioni 657,389 na kuku wa asili na wa kisasa wapatao milioni 83.3.

Mifugo hii huchangia ukuaji wa uchumi na pato la taifa kwa asilimia 7.4, ambapo katika mwaka 2019/2020 sekta ilikua kwa asilimia tano.

Bidhaa zitokanazo na mifugo hasa ngozi katika kipindi cha miaka mitano ya Rais Dk.John Magufuli imepiga hatua ikiwa ni kuimarika kwa soko la bidhaa.

Kuimarika kwa soko kumewabainisha kuanzishwa kwa viwanda ikiwemo kiwanda cha karanga kilichopo Moshi Mkoani Kilimanjaro ambacho kinakubia na Gereza la Karanga na Mfuko wa Hifadhi ya jamii (PSSSF) kwa wafanyakazi wa serikali.

Soko la bidhaa za ngozi imechochea ajira na kuleta uhakika wa kipato kwa wafugaji

Rais Dk.Magufuli Octoba 22 mwaka huu, alishiriki katika ufunguzi wa kiwanda cha Karanga ambapo aliwasisitiza watanzania kupenda na kuthamini bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Alisema kuendelea kutumia bidhaa za ngozi zinazozalishwa nje ya nchi kunadidimiza viwanda vya ndani na kuvifanya kushindwa kuzalisha kwa wingi, hivyo kukosesha serikali mapato na kupunguza wigo wa ajira.

Rais Dk.Magufuli anasema "Kuanzishwa kwa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro kumekuwa na manufaa mengi kwa Taifa ikiwemo kuzalisha ajira nyingi kwa wananchi, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kuongeza wigo na thamani ya soko la ngozi kwa wafugaji.

"Natambua Mkoa wa Kilimanjaro hauna mifugo mingi, mifugo ipo maeneo mengine lakini kwa kudhihirisha ndoto za Baba wa Taifa na kuwapenda wananchi wa Kilimanjaro, Serikali iliagiza kiwanda hiki kikubwa kijengwe hapa Kilimanjaro,"anasema

Mpaka sasa Mkoa wa Kilimanjaro una viwanda vitatu vikubwa vinavyochakata ngozi na kuzalisha bidhaa za ngozi ambavyo ni Karanga Leather,Himo Tanaries(HITA) na Moshi Tanaries.

MTAZAMO WA WADAU.

Mkurugenzi wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Woiso Original Products (WOP) Keneth Woisso anasema serikali ya awamu ya tano imetumia nia mbalimbali katika kunusuru sekta hiyo, ikiwemo kuzuia bidhaa bandia kutoka nje ya nchi jambo ambalo kwa kipindi kirefu lilishindikana.

Anasema kumarika kwa sekta ya ngozi ni nja moja wapo ya kuzalisha ajira hususan kwa vijana na kuwainua wafugaji kwani wanakuwa na uhakika wa kipato, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo soko la ngozi halikuwa la uhakika.

"Tumepiga hatua, hata idadi ya viwanda vidogo vimeongezeka na huu ni mwanzo tu miaka mitano mbeleni, naona mwanga mpya wa matumaini na hakika tutasonga mbele katika sekta yetu"anasema

Anasema kupitia sekta ya ngozi ajira mbalimbali zimekuwa zikipatikana na kutoa fursa za watu kujajiri kuanzia uchunaji ngozi,uchakataji hadi uundaji wa bidhaa mbalimbali bila kusahau wafanyabiashara na wasafirishaji.

Kwa mujibu wa Woisso kilichodumaza soko la ndani la bidhaa za ngozi ni kutopigwa marufuku bidhaa bandia hali ambayo ilileta ushindani usiofaa sokoni huku mlaji akiumia jambo ambalo sasa limedhibitiwa.

Woiso anasema sekta ya ngozi ni mtambuka inazalisha ajira nyingi na kuingiza taifa mapato, hivyo wananchi hawana budi kuunga mkono jitihada zinazofanywa ili kukuza soko hilo kwa manufaa ya taifa.

"Wananchi hawana budi kupenda na kuthamini bidhaa tunazozalisha ili tumarishe soko letu la ndani lakini wakati huo huo tunaenda kuzalisha ajira kwa wingi hususan kwa wale vijana ambao ni mafundi"anasema.

Allen Mshiu fundi viatu anasema, hvi karibuni soko si baya kama ilivyokuwa awali na pia ubunifu kwa wazalishaji umeongezeka na kuwa wakimataifa.

"Soko linakuwa siku hadi siku, mafundi imewalazimu kuwa na ubunifu mkubwa ili kushindana katika soko la kimataifa jambo ambalo linazidi kupanua wigo wa uzalishaji wa bidhaa za ngozi hapa nchini"anasema.

Joivi Shirima mzengenezaji wa viatu mjini Moshi anasema kumarika kwa soko la ndani la bidhaa za ngozi kumesababisha upatikanaji wa malighafi ya ngozi kwa ya uhakika zaidi tofauti na kipindi kingine.

Anasema kutokana na soko kutokuwa la uhakika, wapo baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu walioto'osha ngozi kupitia njia za panya na kwenda kuuza nchi jirani ya Kenya kwa lengo la kupata faida.

JITIHADA ZA SERIKALI

Mwezi Julai 2019 Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alifanya ziara nchini Misri na kukutana na wadau wa sekta ya ngozi nchini humo na kuwaalika kufika nchini kwa ajili ya kuwekeza katika sekta hiyo.

Hata hivyo ziara hiyo ilikuwa na matokeo chanya nchini baada ya wawekezaji kuonyesha nia ya dhati kuhitaji kuwekeza katika sekta hiyo na kukuza moja kwa moja.

Mkurugenzi wa masoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dk.Felix Nandonde anasema wawekezaji wa ngozi walifika nchini kutokana na ziara ya waziri mkuu alipotembelea mji wa viwanda vya ngozi Roubki na kuzungumza na wazalishaji wa bidhaa za ngozi,

Anasema kutokana na uzalishaji unaofanyika nchini humo aliwaalika wafanyabiashara kuja kuwekeza katika sekta ya ngozi kutokana na ubora wa bidhaa zinazopatikana.

"Jambo moja kubwa tumewathibitishia wawekezaji katika sekta ya ngozi kutoka nchini Misri Tanzania ina bidhaa bora za ngozi, wenyewe wamejionea "anasema..

Kuhusu ubora wa ngozi mkurugenzi huyo anasema wizara imejipanga kutoa elimu kwa wachunaji wa ngozi ili kuhakikisha ngozi inayopatikana inakuwa na ubora.

Wananchi hawana budi kupenda na kuthamini bidhaa tunazozalisha ili tumarishe soko letu la ndani lakini wakati huo huo tunaenda kuzalisha ajira kwa wingi hususan kwa wale vijana ambao ni mafundi

VIATU vya ngozi

Scanned with CamScanner

Lengo>> Ni kudhibiti migogoro kati ya wanakijiji na wafugaji

Kijiji chashikilia ng'ombe 250 waliongia bila utaratibu

Na WARIOBA IGOMBE, *Morogoro*

SERIKALI ya Kijiji cha Madaraka Kata ya Doma Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro, inawashikilia ng'ombe 250, baada ya kuingia kijijini hapo kinyume cha utaratibu na kusababisha hofu kwa wakazi wa eneo hilo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Hehema Mandimunam, alisema wamelazimika kukamata mifugo hiyo baada ya mmliki wake, Kelimbeti Mbairo, kuvunja sheria.

"Kijiji hiki kimejiwekea sheria na taratibu ambazo haziruhuru kuiingiza mifugo, hivyo tumelazimika kukamata ng'ombe hawa baada ya mmiliki wake kuingia eneo kwa kuvamia bila kufuata utaratibu na sheria za kijiji zilizopo," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema uongozi uliona ni bora kuchukua hatua hiyo ili kudhibiti athari ambayo ingejitokeza likiwemo suala zima la kuibuka kwa viashiria vya migogoro ya ardhi ndani ya wilaya hiyo.

Hehema alisema kijiji hicho na wilaya hiyo kimekuwa kikiandamwa na migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, hivyo waliamua kuweka sheria ili kulinda amani.

Alisema sheria na utaratibu ambao kijiji hicho kiliamua kuanzisha, migogoro hiyo ingendelea kujitokeza, hivyo kwa kuwa kuna sheria na utaratibu za kuingiza ng'ombe katika kijiji hicho migogoro haipo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, wanawasiliana na uongozi wa wilaya hiyo ili kuangalia hatua sahihi za kumchukulia mmiliki aliyevamia kijiji hicho akiwa na kundi kubwa la ng'ombe bila utaratibu ili liwe fundisho kwa watu wengine.

Hata hivyo, mmiliki wa mifugo hiyo, Mbairo alissema anasitishwa na kitendo cha kushikiliwa mifugo yake kwani hakuwa na lengo baya.

"Kitendo cha mifugo hii kuingia katika kijiji hiki, siyo kwamba kutaibua migogoro ya ardhi kama inavyotafasiriwa viongozi hawa, lakini pia nimefuata taratibu zote zinazotakiwa, hivyo nasikitika kuona mifugo yangu imekamatwa," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Hassan Mjama, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuwa watulivu wakati suala la kuingiza mifugo hiyo bila kufuata utaratibu uliopo, likishughulikiwa kiwilaya.

Scanned with CamScanner

- PICHA:WALTER MGULUCHUMA

MAFANIKIO: Mkazi wa Kijiji cha Ilunde Halmashauri ya Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, Exvery Mwanamahenge akizungumza kuhusu mafanikio ya mradi wa Tasaf yaliyopekelea yeye kununua ng'ombe 8 juzi.

Scanned with CamScanner

- PICHA: WIZARA

MAELEKEZO: Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel (katikati) akielekeza jambo kwa Mhandisi wa Kampuni ya Ujenzi ya Zeco, Gerald Oswald (kulia) alipofanya ziara ya kukagua ukarabati wa bwawa la kunywesheа mifugo la Narakauo Wilaya Simanjiro mkoani Manyara juzi.

Scanned with CamScanner